

MATATIZO YA KUTUMIA KIINGEREZA KUFUNDISHIA KATIKA SHULE ZA SEKONDARI NA VYUO VYA JUU TANZANIA

M. A. S. Qorro

Ikisiri

Makala hii inaeleza matatizo yanayotokana na kutumia Kiingereza kufundishia katika shule za sekondari na vyuo. Makala inaanza kwa kufafanua tofauti zilizopo kati ya kufundisha lugha kama somo kwa lengo la kupanua mawanda ya mawasiliano na kutumia lugha kama nyezo ya kutolea maarifa. Makala imebainisha matatizo ya kijamii, kiutamaduni, kiuchumi, kielimu na kiakili yanayotokana na kutumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia. Katika kubainisha matatizo hayo; makala imetumia vielelezo mbalimbali kutoka kwa walengwa wa viwango tofauti vya elimu; kuanzia kidato cha kwanza hadi chuo kikuu. Makala inahitimisha kwa kupendekeza kuwa ni vema kutumia lugha inayoeleweka; lugha ya Kiswahili, ili wanafunzi waweze kupata maarifa, kisha kutafuta mbinu za kufundisha lugha ya Kiingereza kama somo kwa ufasaha zaidi ili itusaidie katika mambo mbalimbali.

1.0 Utangulizi

Kabla ya kuzungumzia matatizo ya kutumia Kiingereza kufundishia ni vema kupambanua mambo mawili muhimu; nayo ni kutumia Kiingereza kufundishia na kufundisha Kiingereza kama somo. Haya mambo mawili yasipotenganishwa, yakapambanuliwa na kuwekwa bayana mara nyingi yanakanganya mjadala wa lugha ya kufundishia. Kiingereza ni lugha kama lugha nyingine yoyote, na ingawa inabeba mambo mengi lakini kimsingi, ni nyenzo ya mawasiliano. Kufundishwa Kiingereza kama somo ni kujiongezea nyenzo za mawasiliano na watu ambao bila kufanya hivyo ingekuwa vigumu kuwasiliana nao. Kiingereza na Kifaransa ambazo ni lugha za kigeni hapa Tanzania zinafundishwa kwa nia ile ile ya kujiongezea nyenzo na kujipanulia uwanja wa mawasiliano na ulimwengu wa nje. Nchi zote duniani zinafundisha lugha za kigeni kwa malengo hayo kama ya kwetu.

Kutumia Kiingereza kufundishia ni kukifanya kuwa ni nyenzo ya kuwasilisha elimu. Hapa nia siyo kuongeza nyenzo, kama ilivyo katika kufundisha Kiingereza kama somo, bali kuwasilisha maarifa yaliyokusudiwa katika hisabati, historia, jiografia, elimu viumbe n.k. kwa kutumia lugha ya Kiingereza. Lakini ili lugha hiyo ya Kiingereza ikubalike kuitwa nyenzo ya kuwasilisha elimu ni lazima waalimu na wanafunzi waelewe barabara vinginevyo mawasiliano hayo ya elimu hayataweza yafanyika au kukamilika, hali ambayo inazaa matatizo.

2. Matatizo ya kutumia Kiingereza kufundishia

Kuna matatizo ya aina mbalimbali yanayotokana na kutumia Kiingereza kufundishia katika shule za sekondari na vyuo vya juu kwa kuwa lugha hiyo baadhi ya walimu na

asilimia kubwa ya wanafunzi hawaelewi. Baadhi ya matatizo hayo ni ya kijamii, kiutamaduni, kiuchumi, kielimu na kiakili. Nitagusia matatizo haya kwa kifupi.

Matatizo ya kijamii hutokea pale ambapo jamii inaamini kuwa Kiingereza ni elimu na kuwa waliopata elimu (na hasa elimu hiyo inapokuwa katika Kiingereza) ni watu bora zaidi kuliko wale wasiopata elimu hiyo, na kuwa wao pekee ndiyo wenye ujuzi. Mbali na hayo kusomesha vijana kwa kutumia Kiingereza ambayo ni lugha ya kigeni ni njia mojawapo ya kuwasisitizia kuwa lugha yao na elimu katika lugha yao haina thamani, ndiyo maana haitakiwi shuleni. Kwa maneno mengine, elimu ikitolewa kwa lugha ya kigeni kama Kiingereza, inawaandaa vijana kutumikia mataifa ya nje kuliko taifa lao wenyewe. Ipo mifano mingi ya wasomi wa Kiafrika na wa ulimwengu wa tatu ambao wamehamia katika nchi zilizoendelea na kutumikia jamii za nchi hizo badala ya jamii zao ambazo ziligharamia kuwasomesha. Pale wasomi na jamii zao wanapoacha kuthamini mambo yao ya msingi na kudhani kuwa mambo ya kigeni tu ndiyo yenye maana ni tatizo na hasara kubwa kwa jamii hizo.

Matatizo ya kiutamaduni yanatokana na lugha inayotumiwa kushindwa kuhusianisha utamaduni wa kigeni na utamaduni wa Kiafrika. Jambo hili linafanya sayansi na teknolojia kuendelea kubaki nje ya tamaduni zetu kwa kuwa lugha zinazotumika kufundishia hazieleweki kwa wanafunzi na wananchi walio wengi. Matokeo ya hali hii ni kudumaa kwa tamaduni za Kiafrika kwa kuwa hazipati nafasi ya kuchangamana na tamaduni hizo za kigeni, tofauti na tamaduni za Ulaya zilivyopokea sayansi na teknolojia kutoka tamaduni za Wayunani na Wagiriki na kuzimiliki kikamilifu kiasi cha kutufanya sisi tuamini kuwa, kwa mfano Kiingereza ni lugha ya sayansi na teknolojia.

Matatizo ya kiuchumi huwepo pale ambapo siku zote tunaendelea kutegemea mataifa ya nje kutupatia wataalamu, vitabu, na vifaa vya elimu. Gharama za kuagiza vifaa hivyo na kuwalipa wataalamu zikiangaliwa kiuchumi kwa ngazi ya taifa; tukiongezea na matatizo ya kijamii na kiutamaduni yaliyotajwa hapo awali; ni kwamba hata baada ya kugharamiwa kusoma waliosoma watakuwa wanathamini mambo ya wageni zaidi kuliko yale ya kwao. Hii ni hasara kubwa kwa mataifa yanayosomesha vijana wao kwa lugha za kigeni.

Matatizo ya kielimu yanatokea hasa kwa wale wanafunzi ambao hawakielewi Kiingereza na wanalazimika kukitumia kama lugha ya kujifunzia. Utafiti unaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 95% ya wanafunzi katika shule za sekondari nchini Tanzania hawaelewi Kiingereza (Mlama na Matteredu 1977; Campbell na Qorro 1997), kwa hiyo wanashindwa kuelewa masomo yote yanayofundishwa kwa lugha hiyo. Hii ina maana kwamba ingawa serikali na wazazi wanajitahidi kupeleka watoto shule kwa malengo na madhumuni ya kuwapatia elimu, malengo na madhumuni hayo huwa hayatimii kwa kuwa baadhi ya waalimu na wengi wa wanafunzi hawaelewi lugha inayotumika kufundishia, yaani Kiingereza. Kwa maneno mengine, kutumia Kiingereza kufundishia kunapingana moja kwa moja na malengo na madhumuni ya elimu nchini Tanzania.

Aina ya mwisho katika matatizo niliyoyataja ni tatizo la kiakili. Hili ni tatizo ambalo kwa sehemu kubwa halionekani ingawa athari zake zinaweza kuwa kubwa zaidi. Mifano yake

ni pale akili inapozugwa na kufungwa kuamini mambo ambayo wanaotawala elimu watapenda tuyaamini, au pale akili inapokuwa imefunngwa kiasi cha kutoweza kupambanua na kutambua mambo muhimu katika maisha. Tatizo la kiakili linaweza kuwa katika sehemu mbili, yaani: kisaykolojia na uelewa. Katika makala hii nitajaribu kulifafanua tatizo hili kwa undani zaidi kwa kuwa naamini kwamba ndilo tatizo lililozaa yale mengine niliyoyataja.

3. Athari za tatizo la kiakili

3.1 Kisaikolojia (Msimamo na Mtazamo)

Athari kubwa ya tatizo la kisaykolojia ni kutokujiamini ambayo mifano yake ni kama vile kudhani kuwa:

- (i) sisi Waafrika tuna upungufu mkubwa kama binadamu, kwa hiyo kuiga mambo ya wengine ndiyo kunakamilisha utu na ubinadamu wetu;
- (ii) hatukuwa na elimu yo yote mpaka walipokuja wazungu kutuletea kutoka ulaya;
- (iii) utamaduni wetu una hitilafu (ndiyo maana hautakiwi shuleni) kwa hiyo ni wa kuacha na kuchukua utamaduni wa watu wengine;
- (iv) lugha zetu hazina maana wala mchango wo wote katika ulimwengu wa kisasa kwa hiyo kuziendeleza lugha hizo ni kurudi nyuma;
- (v) elimu, sayansi na teknolojia ni mambo ya wazungu kwa hiyo ili tuvipate hatuna budi kuachana na mambo yetu na kuiga yote ya kwao ndipo tutapata maendeleo; na athari nyingine nyingi zitokanazo na kutojiamini.

Hali hii ya kutojiamini inafanya tunakosa pa kuanzia kwa kuwa imetufanya tuyachukie mambo yetu yote; kwa maneno mengine tunaushuku utu na ubinadamu wetu. Yaani hatujiamini kama tu watu kamili, ambao tuna mambo yetu ya msingi yanayodumisha na kuendeleza maisha yetu na uhai wetu. Hali hii ya kutojiamini ni tatizo kubwa kwa kuwa ni kinyume kabisa na matakwa ya maisha ya ulimwengu wa sasa kwamba sisi kama binadamu wengine, tuna mchango mkubwa katika jamii ya binadamu duniani wa kujiletea maendeleo yetu wenyewe. Tutaweza kuleta maendeleo yetu kwa kuanza kujiamini. Kujiamini nako kunahitaji tujithamini na tuthamini mambo yetu, na hasa yale yanayojenga utu wetu. Kwa hiyo ni lazima tujiamini kwanza ili tuchukue nafasi yetu katika ulimwengu ya kujiletea maendeleo yetu wenyewe.

3.2 Uelewa

Tatizo la uelewa linahusiana na lile la kielimu lililozungumziwa hapo awali. Tatizo hili linatokea kwa kuwa wanafunzi walio wengi hawaelewi Kingereza kwa hiyo wanashindwa kuelewa mada ya masomo wanayofundishwa; matokeo yake ni kudumaa kwa uelewa wao kiakili. Kwa mfano tuangalie maandishi ya wanafunzi katika ngazi mbali mbali ya elimu:

Kielelezo cha Kwanza

Kidato cha kwanza, somo la Biolojia

Mada: 'Osmosis':

OSMOSIS

Osmosis is the movement of the solvent from the solution of lower concentration to that of higher concentration through a semipermeable membrane.

Osmosis occurs when two solutions of different concentrations are allowed to pass through a semipermeable membrane. The one which allows some of the material to pass through it.

Example (i) cell membrane (ii) cell wall of plant cell etc.

Solvent is the liquid which is especially used for dissolving solute is water.

Solute is any substance which is mixed with solvent results to the formation of a solution that is it dissolves in solvent.

Solution is the resulting mixture obtained when solvent dissolves in solvent.

Osmotic pressure is the force of osmosis of the solvent across a semipermeable membrane.

Maandishi haya mwanafunzi ameyanakili kutoka ubaoni, na inaonekana kuna maneno ameyanakili visivyo sahihi; k. m. maneno *concentration, through, semipermeable, na of a different concentration*. Hali hii inatoa hisia kuwa mwanafunzi huyu haelewi maneno haya na hana uhakika na muundo wa maneno haya ya Kiingereza bali anaigiza herufi kutokana na jinsi anavyosoma hati ya mwalimu wake. Kwa hiyo mwalimu anapokosea kuandika neno wanafunzi hawana uwezo wa kutambua kwamba kuna tatizo na kuuliza ili kuhakikisha usahihi wake. Vyovyote atakavyoandika mwalimu, wanafunzi hunakili hivyo hivyo. Wakati mwingine ni vigumu kujua kama ni makosa ya mwalimu au ya wanafunzi. Mifano ya makosa kama hayo ni mingi. Yafuatayo ni maandishi ya baadhi ya wanafunzi katika ngazi mbali mbali za elimu (mengine katika Viambatisho), kuanzia Kidato cha pili hadi mwaka wa kwanza chuo Kikuu, katika masomo mbali mbali.

Kielelezo cha Pili:

Kidato cha Pili, Jiografia:

Mada: *Flood Plains*

2. MATURE STAGE OR MIDDLE COURSE OF COURSE OF A RIVER

In the mature or middle stage of the river the following features are found.

1. The valley has the shape of an open V in cross section.
2. The gradient is more gentle than a young valley.
3. River bends are pronounced. The concave banks stand as river cliffs the convex banks slopes (smoothered of spurs)
4. Spurs are removed by lateral erosion. Their remains form a line of bluffs on each side of the valley floor.
5. The valley floor is wide and by the time the valley enters the stages of old age it is covered with a layer of silt.

FLOOD PLAIN

The conditions for bulding a flood plain

1. During maturity the valley floor is widened by lateral erosion which is effected by meanders migrating down stream
2. Active deposition begins to take place on the convex banks of meanders during maturity ultimately the whole valley floor is affected as meanders wander across it.
3. After the stage of maturity is reached river begins to overflow its banks and it deposits fine sand and mud on the valley floor. This is the final stage in the growth of flood plain meanders still.

Kielelezo cha Tatu

Kidato cha Tatu, somo la Biolojia

Mada: Reproduction:

REPRODUCTION

5. It the metabolic process is there by Organism give rise to young Individuals (off spring) of their own kind in order to continue the existence of the species

If there were no reproduction organs present would grow older and die at the end and therefore life would disappear

6. Growth It is the metabolic process where by Organism increase in size and complexity

7. Response – or Irritability or Sensitivity.

It is the ability or power of an organism to react (respond) to different environmental changes called stimuli

All activities that occur internally or externally in an organism are in response to stimuli.

Example of Activities resulting from response are such as seeing hearing smelling tasting – illness etc.

Je kutokana na vielelezo hivi, ni kweli kwamba wanafunzi hawa wananufaika kielimu na kiakili Kiingereza kinapotumika kufundishia? Wanaodhani wanafunzi wananufaika ni vema wakatoa vielelezo vinavyoonyesha kunufaika huko. Lililo dhahiri katika maandishi ya wanafunzi hawa ni kwamba hali hii ya kutumia Kiingereza kufundishia inawanyima elimu wanafunzi wengi. Katika kunakili maneno ambayo hawayaelewi, wakati mwingine wanafunzi wanayanakili vibaya kiasi cha kupotosha kabisa maana ya neno. Kwa mfano neno ‘monder’ (kielelezo cha Tatu mstari wa 3) ilipaswa kuwa ‘in order’

lakini mwanafunzi amechanganya herufi ‘i’ na ‘n’ kuwa herufi ‘m’. hali hii inaweza kutokea mwanafunzi anapokuwa hawezi kutofautisha ‘in order’ na ‘monder’ na hatambui kwamba neno ‘monder’ halina maana yoyote katika Kiingereza. Maneno mengine yaliyokosewa katika kielelezo cha Tatu peke yake ni:

- ‘metabolis’ badala ya ‘metabolic’ (mstari wa 2)
- ‘organium’ badala ya ‘organism’ (mstari wa 6)
- ‘insleal’ badala ya ‘increase’ (mstari wa 6)
- ‘scnsolivity’ badala ya ‘sensitivity’ (mstari wa 7)
- ‘obitily’ badala ya ‘ability’ (mstari wa 8)

Haya ni baadhi tu ya makosa (na mengine mengi kama inavyooneshwa katika vielelezo vilivyotumika) wanayofanya wanafunzi kati ya asilimia 70% hadi 75% katika shule za sekondari hapa nchini (Qorro 1999). Katika hali hii, je ni kweli kwamba wanafunzi hawa wanajifunza Kiingereza ati kwa kuwa kinatumika kufundishia? Mimi nina mashaka makubwa na hali hii, na ninaamini kuwa wanafunzi wakitumia maneno kimakosa kwa muda mrefu wakaamini kuwa ndivyo yanavyoandikwa, baadaye inakuwa vigumu kusahihisha makosa haya ambayo watakuwa na uzoefu nayo katika akili zao. Hali hii inafanya kazi ya mwalimu wa Kiingereza kuwa ngumu zaidi ya kuwatoa katika makosa haya yaliyozoeleka na kuwafundisha maneno na lugha sahihi. Hali hii huenda ndiyo moja ya sababu zinazofanya kazi hii ya kufundisha Kiingereza kuwa ngumu kwa walimu wa somo hili katika ngazi zote za elimu.

Inaelekea kuwa sote tunaamini kwa nia njema kabisa kwamba kwa kutumia Kiingereza kufundishia wanafunzi wanapata uzoefu wa lugha hiyo. Hii ni kweli katika hali ya kawaida. Lakini hali halisi katika shule zetu, kama inavyodhihirishwa na vielelezo tulivyoviona, inaonesha kwamba si ya kawaida; tunachodhani kipo, kumbe kweli hakipo. Badala yake kipo kibovu kabisa, na wanaopaswa kukitumia hawakielewi. Je tuendelee kufundishia hicho hicho kibovu? Kuendelea na hicho kibovu imedhihirika kuwa na athari mbaya zaidi kwa watoto wetu. Athari za kukosa elimu, kuzoea Kiingereza kibovu na ugumu wa kukirekebisha wanafunzi wafikapo elimu ya juu, pamoja na athari nyingine za kijamii, kuuchumi, zilizotajwa awali.

Vielelezo hivi vinathibitisha hoja ya wanafunzi kukosa uelewa, ambayo ni moja ya matatizo ya kutumia Kiingereza kufundishia. Tatizo hili linajitokeza kwa kuparanganya ukweli wa mambo yalivyo, yaani wanafunzi kutoelewa mambo wanayopaswa kuyaelewa. Kwa mfano, katika kielelezo cha pili maana ya neno *meanders* imeparanganywa. Kwa kusoma maadishi hayo utadhani *meanders* ni vitu vinavyosafiri katika mto, au vinasombwa na mto. Matokeo ya tatizo la wanafunzi kutoelewa dhana muhimu katika yale wanayofundishwa ni kudumaa kwa uelewa katika ujumla wake. Vielelezo tulivyoona pia vinathibitisha uelewa finyu wa wanafunzi katika shule zetu, yaani, wanafunzi kuwa na uelewa mdogo sana wa mambo mengi yanayofundishwa shuleni. Ipo mifano mingi ya namna hii katika shule na vyuo vyetu na inaweza kuonekana katika kazi za wanafunzi wa ngazi mbalimbali za elimu hapa nchini (tazama Viambatisho). Kinyume cha hali hii ni uelewa mpana unaowawezesha wanafunzi kutambua mambo, kuuliza maswali, kushiriki katika kujadili masuala mbalimbali ya masomo yao na kujifunza kutatua matatizo. Yaani kile Cummins (1979, 1981) alichokiita “Cognitive Academic

Language Proficiency” au kwa kifupi ‘CALP’, ambayo ni hali ya kukua au kupanuka kwa uelewa wa wanafunzi, hali ambayo inawapa misingi au uwezo wa kuwa na uelewa mkubwa zaidi wa kujifunza mambo kwa kina na mapana. Hali hii ya uelewa mpana ni haba sana katika shule na vyuo vyetu.

Matatizo haya kwa pamoja yanasababisha wanafunzi kutokuwa na uelewa barabara wa mambo wanayofundishwa, kwa hiyo wanashindwa kusimama kidete kutetea hoja zozote katika masomo yao kwa kuwa hawajaelewa au hawana uhakika wa yale waliyoyasoma au kuyasikia, au hawajiamini kwa kukosa uelewa huo. La muhimu zaidi, wanakosa misingi ya uelewa wa mambo mapya katika ngazi za juu za elimu au katika maisha baada ya kumaliza shule. Kwa kuwa misingi hiyo haijajengwa wanapokuwa shuleni. Shule inaelekea kuwa ni mahali pa kupotosha badala ya kunyoosha dhana za kielimu. Hali hii ya kukosa uelewa wa mambo yaliyofundishwa inawafanya washindwe kujifunza.

Ili kujifunza lugha binadamu anahitaji kufanya mazoezi ya kumweleza binadamu mwenzake jambo alilionalo akilini. Iwapo kwa kufundishwa masomo mengine kwa Kiingereza wanafunzi hawakuelewa, yaani mada iliyofundishwa haikuingia akilini mwao hali hiyo inawapunguzia uwezo wao wa kujifunza Kiingereza kwa kukinyima uwanja wa mazoezi. Lugha ni nyenzo tu ya kuwasilisha maudhui yaliyoko katika akili ya mtu, endapo maudhui hayajaingia akilini, yakaeleweka, nyenzo (lugha) inakuwa haina cha kuwasilisha katika yale yaliyofundishwa, kwa hiyo wanafunzi wanakosa jambo la kuzungumza, wanakuwa kama wamefungwa kauli. Tumeshuhudia hali hii wakati wanafunzi wetu wanaposhindwa kueleza hata kwa Kiswahili au lugha zao za awali mambo waliyojifunza shuleni kwa kuwa mambo hayo waliyofundishwa hayajawaingia akilini.

4. Hitimisho

Kama ilivyoelezwa mwanzoni mwa makala hii, kufundisha Kiingereza kama somo na kutumia Kiingereza kufundishia ni mambo mawili tofauti. Tunaweza tu kufanikiwa kutumia Kiingereza kufundishia iwapo wanafunzi wanaelewa Kiingereza. Kuendelea kuamini kwamba wanafunzi watajifunza Kiingereza iwapo kitatumika kufundishia katika hali ilivyo sasa ni kuendelea kujidanganya na kutafuta njia za mkato. Tunajidanganya kwa sababu mara nyingi Kiingereza wanachokisikia shuleni na mitaani ni kibovu au si fasaha. Kiingereza fasaha kimebaki kuwa lugha ya wachache tu katika shule zetu. Kwa walio wengi Kiingereza kinaendelea kuwa lugha ngeni. Kufundisha jambo geni kwa kutumia lugha ngeni ni sawa na kutaka kufumbua fumbo ambalo halina ufumbuzi na halifumbuliki. Ni vizuri tukatambua kuwa hatuwezi kukamilisha mambo haya mawili, yaani kuwapa wanafunzi elimu na kufundisha Kiingereza kwa njia moja ya mkato, yaani kutumia Kiingereza kufundishia. Badala yake tuwape vijana elimu kwa lugha wanayoelewa, wakishaelewa, ile hali ya kuelewa iwasaidie kujifunza mambo mengine mapya (pamoja na Kiingereza) ili taifa lijikwamue kutoka katika matatizo ya kijamii, kitamaduni, kiuchumi, kielimu na kiakili pamoja na athari za matatizo haya kama ilivyoelezwa katika makala hii.

Tunapoendelea kuamini kwamba wanafunzi wanajifunza Kiingereza kinapotumika kufundishia, (yaani kuua ndege wawili kwa jiwe mmoja) tunadhani hakuna umuhimu wa kutafuta mikakati ya kufundisha Kiingereza vizuri. Tunajituliza kuwa 'watajifunzia humo humo'. Kwa hiyo tatizo letu kubwa ni kwamba hatulizungumzii tatizo lenyewe, badala yake tunalumbana kuhusu lugha gani itumike kufundishia. Tukiendelea kubishana watoto wetu wanakosa vyote: yaani elimu, Kiingereza na hata Kiswahili. Vielelezo viko vingi vinavyodhihirisha hali hii ya kukosa vyote. Lugha ya kufundishia haipaswi kuwa suala la mjadala, kwa kuwa siku zote na mahali pote mtu hufundishwa kwa lugha anayoelewa. Kwa hiyo tuliweke kando ili tutafute namna ya kutatua tatizo lenyewe, yaani kufundisha Kiingereza vizuri kama somo. Ninaamini kabisa kwamba wanafunzi tukiwafundisha kwa lugha wanayoelewa, yaani Kiswahili, wataweza kupata elimu, kuimarisha uelewa wao ambao utawaongezea uwezo wa kujifunza mambo mengi na kwa undani zaidi. Kwa maana nyingine wataepuka kwa kiasi kikubwa matatizo tuliyoyataja yanayotokana na kutumia Kiingereza kufundishia katika shule za sekondari na elimu ya juu.

Marejeo

- Cummins, J. (1979) 'Cognitive/Academic Language Proficiency, Linguistic Interdependence, the Optimal Age Question and Some Other Matters', *Working Papers on Bilingualism*, 19, 197-205.
- Cummins, J. (1981) 'The Role of Primary Language Development in Promoting Educational Success for Language Minority Students' in *Schooling and Language Minority Students: A Theoretical Framework*, 3-49.
- Mlama, P. and Matheru, M. (1977) 'Haja ya kutumia Kiswahili kufundishia elimu ya juu', Dar es Salaam: BAKITA.
- Roy-Campbell and Qorro, M. (1987) 'A Survey of the Reading Competence in English among Secondary School Students in Tanzania', a Research Report funded by IDRC.
- Roy-Campbell and Qorro, M. (1997) *The Language Crisis in Tanzania: the myth of English versus Education*, DSM: Mkuki na Nyota Publishers.

Viambatisho

Kidato cha Tatu, Historia

Mada: 'Expansion of State System'

By the end of 18th some of the states had become big centralized kingdoms. By the middle of 19th C states such as Buganda, Bunyoro, Ankole, Rwanda and Burundi had become powerful through trade and military conquest.

The relation of production in the states was feudal. The forms of these relations varied from one area to another in the interlacustrine area the power holder was based on his ownership and control over land the major means of production. The ruling classes (feudal lords) apportioned arable land to the peasants. From the feudal lords collected tribute. The Nyarubanja system in Karagwe, and Nyunjo and Busolo system in Buganda were variations of these feudal relations. Another form of feudal relation was Ubagabice which developed between the Tutsi and Hutu in Rwanda, Burundi, and Buha. Here feudal relations revealed cattle ownership. The Tutsi would own some of the cattle of the Hutu family. Land lord (master) owned cattle and his subject was called Mugabbi i.e.

Kidato cha Tano, Somo la Fasihi katika Kiingereza (Literature in English)

Mada: The Play by Dedan Kimathi

The play tries to reveal to us the relation or contact between whites and blacks. They use their main character to show how the whites treat the blacks (African). We see that through the themes which are discussed in this play. The play of Dedan Kimathi written by Micere Mugo and Ngugi wa Thiong'o.

Themes which are discussed are Racial discrimination: This is shown

Through the use of Italics (pg 3) OPENING "Africans squeeze around one side seated on rough benches, whites occupy more comfortable seats on the opposite side"

Oppression: the boy tells how his father is chased away from mbari land in Njeri by one of his relatives who worked as a court official

Mwaka wa Kwanza, Chuo Kikuu Somo la Kilimo

Mada: 'Releasing an innovation too soon or too late'

The releasing of an innovation too soon or too late causes some consequences such as – the society is not aware of the innovation. That means the ignorance of the society. For example, for the simple farmers which have not used a computer to manage their farm – cannot get any problem of the use of computer. Therefore it is no sense to release too soon these techniques to them.

The cost of the innovation is also a factor ... need to delay the releasing of the innovation. The management of the innovation should require a qualified agent to bring

it to the farmer because the farmers need a very (strong) convincing method or innovation to make them to adopt. For the case that the farmers have got a real problem such as the spread of pests the s... of the innovation should be applied at the time so that it

Its importance and the success either toward the farmers' attitude or the use of the technique.

Another consequence is the reject of the curr... production if the innovation is late to reach targeted farmers. For examples the yield of crop is reduced due to the lack of a mineral. The supply of fertilizer to compensate this lack, is not available. Hence Farmers leave the cotton production for another crop-production